Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 26 JANUARI, 2010

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijatoa Taarifa ya Spika, mtakumbuka tarehe 31 Desemba, 2009 tuliondokewa na Mzee wetu Rashidi Mfaume Kawawa. Mzee huyu amefanya kazi katika Bunge muda mrefu sana na kiasi kikubwa ndiye aliyekuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali ndani ya Bunge. Kwa mujibu wa taratibu zetu na kanuni tulizojiwekea na mazowea, nakuombeni tusimame kwa dakika moja ili tuweze kumkumbuka Marehemu.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, Marehemu Rashid Mfaume Kawawa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana, tunamwomba Mwenyezi Mungu, Mwenye rehema kwa ajili ya maisha ya Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aiweke Roho yake mahali pema peponi Amina.

Waheshimiwa Wabunge, sasa natoa taarifa kwamba katika Mkutano wa Mkutano Kumi na Saba, yaani uliopita, Bunge lilipitisha Miswada minne ifuatayo ya Sheria: *Cashewnut Industry Bill* ya 2009, *The Cereals and Other Produce Bill ya 2009, The Crops Laws Miscellaneous Ammendment Bill ya 2009,and The Law of the Child Bill, 2009.* Mara baada ya kupitishwa na Bunge na baadae kupitia katika hatua zake zote za uchapishaji, Miswada hiyo ilipelekwa Kwa Mheshimiwa Rais wetu ili kupata kibali chake.

Kwa taarifa hii, nashukuru kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu kwamba, tayari Mheshimiwa Rais ameridhia kwamba Miswada hiyo iwe Sheria na sasa ni Sheria za Nchi kama ifuatavyo:-

*The Cashewnut Industry Act*, 2009 unakuwa Sheria Namba 18 wa Mwaka 2009; *The Cereals and Other Produce Act*, 2009 inakuwa ni Sheria Namba 19 ya Mwaka 2009; *The Crops Laws Miscellaneous Ammendment Act*, 2009 sasa ni Sheria Namba 20 ya

Mwaka 2009; na *The Law of the Child Act,* 2009 sasa ni Sheria yetu Namba 21 ya Mwaka 2009.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Uratibu wa Mambo ya Maafa Baharini

**MHE. MWAKA ABBULRAHAMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi iwapo yatatokea maafa ya baharini katikati ya Tanzania Bara na Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, maafa hayana mpaka wala kiwango. Maafa ni tukio na tatizo linaloweza kutokea wakati wowote, hivyo ni muhimu kukawa na ushirikiano kati ya wadau mbalimbali juu ya namna ya kujihadhari na kuchukua hatua mara moja janga linapotokea.

Mheshimwa Spika, Sera ya Taifa ya Udhibiti wa Maafa ambayo ilipitishwa na Serikali mwaka 2004, inasisitiza kuwepo kwa ushirikiano wa Kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Umoja wa Nchi Huru za Afrika, Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kimataifa kwa ujumla, ambapo kuna msisitizo mkubwa wa kuzitaka Nchi Wanachama kuweka utaratibu mzuri wa kukabiliana na maafa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maafa ya baharini kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kama yaliyotokea tarehe 29 Mei, 2009 saa 3.45 usiku, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zetu mbili zimejipanga vizuri kukabiliana na maafa kama hayo.

Kulingana na mgawanyo wa majukumu ya kukabiliana na maafa, Asasi Ongozi ambazo ni Jeshi la Majini *(Navy)* na Polisi Kikosi cha Majini *(Marine Police)*, kwa kushirikiana na SUMATRA na wadau wengine, wamepatiwa mafunzo na nyenzo za kisasa na wanafanya mazoezi kwa vitendo ya jinsi ya kukabiliana na dharura za baharini.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza uwezekano wa ajali kutokea, ukaguzi wa mara kwa mara unafanywa na vyombo kama meli, majahazi, mitumbwi mikubwa na kadhalika, vinavyosafiri baharini. Aidha, wamiliki wa vyombo kama hivi wametakiwa kisheria kuhakikisha usalama wa vyombo vyao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Rajab halafu Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa ulinzi wa baharini hivi sasa umeimarishwa vizuri sana lakini hakuna aina yoyote ya mtandao uliowazi kwa wale wanaopata maafa ili waweze kuutumia na kupata msada wa haraka; Waziri anasemaje katika hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimjibu Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, swali lake la nyongeza kama ifutavyo:-

Ni kweli kabisa kwamba, kwa sasa ulinzi wa baharini umeimarishwa kabisa hasa kwa sababu ya ugaidi ambao unaendelea hivi sasa katika Pwani ya Afrika ya Mashariki.

Kuhusu fidia kwa walioathirika katika ajali iliyokea mapema mwaka huu, tunaamini kwamba mwenye chombo kile amekiwekea Bima na hivyo waathirika wote wanatakiwa wafuate utaratibu wa kawaida wa malipo kwa kutegemea na Bima iliyokewa chombo kile.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumuulizaMheshimiwa Waziri swali dogo kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Nchi ya Haiti imepata maafa makubwa sana ya tetemeko la ardhi na watu wengi sana wamefariki na nchi nyingi Duniani zimejitolea kuisaidia nchi hiyo; je sisi Tanzania tumejiweka vipi kuisaidia nchi hiyo?

**SPIKA:** Nadhani kilichokuwa kinaulizwa hapa kinahusu maafa yanayotokea baharini na hususan fukwe kati ya Tanzania Bara na Visiwani. Nadhani hilo ni swali zuri sana lakini lipatiwe wakati wake.

Swali linalofuata sasa linaelekezwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na linaulizwa na Mheshimiwa Diana Chilolo.

Na. 2

**Ujenzi wa Kituo Kipya cha Polisi Wilaya ya Manyoni**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi la polisi Wilaya ya Manyoni halina Ofisi ya kudumu na yenye hadhi ya Wilaya; na kwa kuwa ofisi ndogondogo zilizopo hazijakarabatiwa hadi sasa licha ya Serikali kuahidi kufanya hivyo; na kwa kuwa Serikali ilishaamua kujenga Kituo Kipya cha Polisi cha Wilaya:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga Kituo hiki kipya cha Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimia Diana Mkumbo Chilolo kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba, kati ya Wilaya tatu za Mkoa wa Singida, Wilaya yenye kituo ambacho kina hadhi ya Kituo cha Polisi cha Wilaya ni Singida pekee. Polisi katika Wilaya za Manyoni na Iramba, wanatumia majengo yaliyoazimwa kutoka Halmashauri za Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kujenga Vituo, Ofisi za Kudumu na zenye hadhi katika kila Mkoa na Wilaya hapa nchini, hata hivyo nia hiyo inakwamishwa na upatikanaji wa fedha. Hatua tuliyofikia kwa sasa katika ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya ya Manyoni ni kupatikana kwa kiwanja cha ekari 20 ambazo zimepimwa tayari kwa ajili ya kujenga Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Manyoni, Kituo cha Polisi na Makazi ya Askari. Ujenzi haujaanza kwa sababu fedha hazijapatikana.

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri kupatikana kwa fedha za kujenga Ofisi hiyo, Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Manyoni wameanza kufyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Askari wa Wilaya ya Manyoni kwa kutumia mashine ya kufyatulia matofali ya bei nafuu, ambayo ilitolewa na Mheshimiwa John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa swali hili nimeshauliza mara nyingi hapa Bungeni huu mwaka ni wa nne; na kwa kuwa kila ninapojibiwa ni hali ngumu ya kifedha; na kwa kuwa hata Mbunge wa Jimbo kwa kuonesha umuhimu wa suala hili ameamua kujitolea fedha zake mwenyewe kuanzisha ujenzi huo; je, Serikali haiwezi kunihakikishia kwamba kupitia Bajeti ya mwaka huu fedha za kujenga Kituo hiki zitatengwa?

(ii) Kwa kuwa Miradi ya Serikali ya Nchi yetu huwa inatekelezwa kwa mpango shirikishi; na kwa kuwa hata jamii inaweza kutoa mchango wake iwapo itashirikishwa; je, Serikali inashirikisha vipi jamii kuunga mkono suala hili ambalo lina uzito mkubwa ukizingatia kituo hicho cha polisi kiko *mortuary* eneo ambalo maiti zillikuwa zinakaa hata mizimu hiyo bado inawashtuashtua maaskari waliopo hapo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili suala ameliuliza mara kadhaa hapa Bungeni. Nadhani ni bora kukwambia ukweli kuliko kukwambia uongo halafu tukaja tukasumbuana; ukweli wa mambo ni kwamba, bajeti yetu ina matatizo na ningeweza tu nikampa picha halisi ilivyo kwa kujibu suala lako na hili ni suala ambalo Wabunge wengi wanaliuliza hapa ndani ya nyumba hii. Vituo vya Wilaya tulivyonavyo katika Tanzania nzima viko 146 na kati ya hivyo 146 nilivyovitaja, Manyoni na Iramba vinaingia katika vituo ambavyo havijakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Tarafa katika Tanzania nzima viko 493 na sikwambii sasa katika ulinzi shirikishi ambapo tunazungumzia kujenga Vituo vya Kata ambavyo vipo 2068. Sasa unakuta huwezi ukasema kwamba katika Bajeti hii nikupe uhakika, isipokuwa ninachosema ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, inawalinda Wananchi wake na kuona kwamba huduma hii inafikishwa kwa Wananchi; na hiyo tunafanya na niseme tu kwamba, suala la Mheshimiwa Mbunge tunalo na tunazidi kulitazama katika bajeti yetu na pale ambapo itaruhusu lakini si Bajeti tu hata ambapo tunapata misaada toka kwa wahisani.

Mheshimiwa Spika, suala lake la pili Mheshimiwa Mbunge nitajibu kwamba, tunakwenda katika njia hiyo ya kushirikisha jamii, kushirikisha wananchi. Kwa kweli tumepiga hatua na ninadhani ni matumaini yangu kuwa, kupitia katika njia hiyo vituo vingi kikiwemo kituo hiki vitakamilishwa. Nakuomba Mheshimiwa Mbunge uelewe hali halisi tuliyonayo katika nchi yetu.

**SPIKA:** Maswali mawili mafupi sana ya nyongeza, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel na Mheshimiwa Mgana Msindai.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo lililoko katika Wilaya ya Maswa, Mkoa wa Shinyanga, linafanana na tatizo lililoko katika Mkoa wa Singida; na kwa kuwa Wilaya ya Maswa wanatumia pia majengo ya kuazima ya Halmashauri; na kwa kuwa sasa hivi Wananchi wa Wilaya ya Maswa wamejitahidi kufyatua matofali na kuchimba msingi; Serikali inasemaje au Wizara inasema nini juu ya uchangiaji wa Kituo hiki cha Polisi Wilaya ya Maswa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika suala na jibu langu la msingi nimeeleza hali halisi tuliyokuwa nayo, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika njia hii ambayo tunakwenda nayo ya kuhamasisha Wananchi na kuwashirikisha, nadhani tutapiga hatua na tunaweza kukamilisha azma ya kuweka kituo hicho.

Ningekuomba tu ni kiasi cha kutuelewa, siyo kwamba iko nia mbaya, nia ni nzuri ila uwezo mdogo unatupa tatizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgana Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Kwa kuwa Wananchi wa Iramba Mashariki walishajenga Kituo cha Polisi pale Nduguti na kimekamilika na Serikali iliahidi kuleta vifaa vinavyotakiwa; je, Waziri atasaidiana na mimi kutafuta hivyo vifaa ili tuwape Wananchi wa Iramba Mashariki wapate huduma nzuri ya polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ipo tayari kushirikiana na yeye katika kuona kuwa tunafanikisha jitihada za kupata vifaa hivyo ambavyo viliahidiwa katika Kituo cha Polisi alichokitaja. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Wizara hiyo hiyo, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda kwa niaba ya Mheshimiwa Dewji.

Na. 3

**Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Polisi Somanga**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI (K.n.y. DKT. SAMSON FERDINAND MPANDA)** aliuza:-

Kwa kuwa Kituo Kidogo cha Polisi cha Somanga Kata ya Kinjumbi kilichojengwa na Wananchi na wahisani mbalimbali kimekamilishwa kwa 75%: Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao kukamilisha kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Samson Ferdinand Mpanda, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu na TAMISEMI, ina mpango wa kujenga vituo vya polisi na nyumba za kuishi askari katika Kata kwa kuwashirikisha Wananchi kusogeza huduma ya kipolisi karibu na Wananchi.

Mpango huu utaanza katika mwaka wa fedha ujao (2010/2011), kwa kuanzia ujenzi katika sehemu ambazo zinahitaji huduma hiyo kwa sababu ya matishio ya uhalifu, lakini pia kwa uamuzi wa Wananchi wa eneo husika kwa dhamira ya kuhitaji huduma za kipolisi. Kupitia utaratibu huu, hatimaye maeneo mengi yatapata huduma za kipolisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Somanga, Kata ya Kinjumbi, Uongozi wa Polisi utaanza mawasiliano na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Lindi katika kubaini mikakati ya kuhakikisha kuwa Ujenzi wa Kituo hicho inakamilika.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Dewji.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, sambamba na tatizo la kituo pale Somanga kuna matatizo makubwa katika ulinzi wa Bahari; je, Serikali ina mpango gani kuweka maboti maeneo ya Somanga ili kunusuru maharamia wanaoteka vyombo mbalimbali vinavyopita pale na kutia hasara kubwa sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ulinzi ni wa Taifa letu kwa ujumla na unaohusu Jeshi la Polisi, lakini na Wananchi pia, ndiyo maana nazungumzia ulinzi shirikishi.

Kuhusu ulinzi katika eneo la Bahari, kwa kweli tunafanya na sasa hivi tuko katika mkakati na tutakuja kuizungumzia hapo baadae juu ya vifaa ambavyo tumevipata vya maboti na kutazama tutafanya doria kwa njia zipi katika kuimarisha ulinzi katika maeneo haya. Itakuwa vizuri Mheshimiwa Mbunge baada ya maswli na majibu tuzungumze nikueleze ni vipi tutafanya.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Job Ndugai halafu Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Kibaigwa katika Wilaya ya Kongwa, walijitahidi wakajenga Kituo cha Polisi, baada ya kujenga wakaambiwa lazima wajenge nyumba ya Mkuu wa Kituo na wakajenga; baada ya pale wakaambiwa samani za kituo lazima wao wahangaikie wakajitahidi wakatengeneza samani za kituo cha polisi na sasa hivi wanachangia kupatikana kwa pikipiki kwa ajili ya kusaidia polisi hao na kuna gari pale; sasa panapotokea matukio wananchi wanaambiwa wachangie dizeli ya gari la polisi na majuzi wananchi hawa walichangia matairi ya gari la polisi; sasa swali langu ni kwamba hivi bajeti tunayotenga hapa Bungeni inafika huko chini?

Je, hili la kuchangia mafuta kwa ajili ya matukio ili magari ya polisi yaweze kwenda kule nalo linakubalika kwamba ni mchango wa wananchi nao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, masuala ya ulinzi na usalama wa Taifa letu kwa kweli ningeshauri si kitu cha kwenda hadharani sana na zipo sababu za msingi wala siyo kwamba kuna kificho hapa, isipokuwa

sidhani kama kitu bora kuanza kwenda hadharani kuzungumza madhaifu ambayo tunayo katika maeneo fulani fulani ya ulinzi wetu.

Nadhani tunaweza kuzungumza na tunaweza kufikia pahala na hali halisi ikaeleweka. *Of course*, Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakaliona kwamba hilo ni jambo jepesi, lakini tunapokuja kupatwa na mambo yaliyokuwa makubwa inatokana na jinsi tulivyojipanga katika nguvu zetu ama katika udhaifu wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali la Mheshimiwa Ndugai ni kwamba, si sahihi wananchi kuchangia dizeli ama kununua matairi ya gari kama alivyotamka. Kwa kuwa amelitaja hili, tutalitizama na tutajua ni kwa nini hii inafanyika, lakini niseme kwamba si wajibu wa wananchi kuchangia vitu kama mafuta ama vitu kama matairi ya gari, lakini pia nataka niseme kwamba si vizuri maana kuna mahala ambapo tunaweza tukazungumzia majambo haya kuliko katika hadhara namna hii.

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyaa umepoteza haki yako ya swali. Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kwa ruhusa yako niwatakie wenzangu wote heri ya mwaka mpya na kuwapa pole waliopatwa na maafa mbalimbali.

Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba hiyo taarifa anayosema ni ya siri katika Report ya CAG imo na siyo siri na taarifa hiyo imo kwenye Bunge hili; na kwamba tatizo la msingi ni kuwa tumewataka Wananchi wasaidie wananchi wamechangia kwa kiasi fulani; huoni kwamba Wizara bado haijajipanga vizuri pale ambapo Wananchi wamesaidia namna gani inaweza ika-*intervene* ili kuondoa haya matatizo ambayo unaona ni aibu kuyasema katika Bunge hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninapozungumzia usiri wa jambo ipo tofauti, kitu kinapozungumzwa na mtu na kitu kinapozungumzwa na mtu aliyekabidhiwa dhamana ya kitu kile.

Ninapozungumza juu ya usiri sijazungumzia kuwa kuna mambo ya kuficha hapa, isipokuwa siwezi kwenda bayana nikazungumzia juu ya udhaifu fulani tulionao katika hali ya ulinzi wa nchi yetu haiwezekani na popote Duniani ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo nimesema na nitarejea tena ni kweli tunazungumzia juu ya ulinzi shirikishi, tunazungumzia juu ya kuwahamasisha wananchi nao washiriki katika kuchangia maendeleo yao katika maeneo mbalimbali hata katika eneo la ulinzi.

Nimetamka hapa kwamba, si sahihi wananchi kuchangishwa kwa ajili ya kununua diesel au matairi na kadhalika; hilo nimekiri na nimesema tutazama katika eneo hilo kujua tatizo liko wapi na kwa nini kimetokea.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na maswali kuelekea Wizara ya Fedha na Uchumi, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja mwanaume amekaa kiti cha Mheshimiwa Esther Nyawazwa, lakini pia amekuwa na hamu sana ya kuuliza swali nimeshindwa kumtambua kwa sababu ukiwa hapa mezani inakuwa vyepesi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika ni mimi mwenyewe.

**SPIKA**: Aah, samahani sana Mheshimiwa Nyawazwa nakuomba radhi. (*Kicheko*)

Na. 4

**Kusimamishwa kwa Malipo ya Pensheni ya Wastaafu**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA (K.n.y. MHE. CASTOR R. LIGALLAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna baadhi ya wastaafu ambao walikuwa wanalipwa pensheni zao mpaka Januari 2008 bila matatizo na ghafla malipo yakasitishwa baada ya mwezi Februari 2008:-

(a) Je, ni nini kimetokea kwa Wastaafu hao?

(b) Je, ni lini zoezi la kuhakiki wastaafu hao litafanyika Serikalini kama PPF ilivyofanya hivi karibuni kwa Wastaafu wanaolipwa na Mfuko huo?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya Wastaafu hao waliosimamishiwa malipo yao ya pensheni akiwemo na Hamis M. Kasungura, PEN/CHECK NO. 51755/15, Benki Account: 7070051755?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mhehsimiwa Castor Raphael Ligallama , Mbunge wa Jimbo la Kilombero, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 31/01/2008 hadi 15/03/2008, Serikali imechukua hatua ya kuwahakiki Wastaafu wote wanaolipwa na Hazina. Hatua hiyo imekuja baada ya Serikali kufanya uamuzi wa kuwalipa Wastaafu pensheni kupitia kwenye akaunti zao za benki. Wastaafu ambao hawajajitokeza katika zoezi la uhakiki, Hazina imeyaondoa majina yao kwenye orodha ya wanaolipwa pensheni na kusimamisha malipo yao hadi hapo watakapojitokeza kwa uhakiki.

(b) Mheshimiwa Spika, zoezi la kuwahakiki Wastaafu wanaolipwa na Hazina limeshafanyika na Serikali inatarajia kufanya zoezi lingine la uhakiki mwishoni mwa mwaka 2010 au 2011.

(c) Mheshimiwa Spika, Wastaafu waliosimamishiwa malipo yao akiwemo Bwana Hamisi M. Kasungura, wanatakiwa kuhakikiwa kwanza kabla ya kurejeshwa kwenye daftari la walipwa pensheni. Wastaafu hao wanatakiwa kufika Ofisi za Hazina Ndogo zilizopo Mikoani mwao au Hazina Makao Makuu, Dar es Salaam au Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar, kwa ajili ya kuhakikiwa wakiwa pamoja na nyaraka zifuatazo:-

(i) Picha ndogo sita za rangi (*passport size*);

(ii) Kitambulisho chake cha pensheni;

(iii) Barua ya tuzo la kustaafu;

(iv) Nakala ya hati ya malipo ya pensheni (*payment voucher*);

(v) Barua ya ajira ya kwanza;

(vi) Barua ya kustaafu au kupunguzwa kazi;

(vii) Kitambulisho chake au *passport;* na

(viii) Taarifa ya akaunti yake binafsi ya benki.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, hakuna mstaafu atakayekosa haki yake, cha muhimu ni kuwepo kwa kumbukumbu sahihi ili taratibu za kulipa pensheni ziweze kuheshimiwa na kufuatwa pamoja na kuwasaidia wakaguzi katika kazi yao ya uhakiki.

**MHE. CLEMENCE K. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kuuliza swali lifuatalo: Kwa kuwa waliokuwa Watumishi wa Mashirika ya Umma ya Serikali wengi inaelekea kuna ucheleweshaji mkubwa wa kulipwa pensheni zao za kila mwezi hususan pamoja na Kilombero Sugar Company; je, Serikali inatambua hili na inachukua hatua gani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, nataka nieleze kwa kifupi tu kwamba, Watumishi wa Umma wapo ambao wanalipwa pensheni zao kupitia Hazina na wapo ambao wanalipwa fedha zao kupitia *PPF*.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kulipwa kwa pensheni nataka nithubutu kusema kwamba, kumepungua kwa kiwango kikubwa kwa sababu wengi wao wanalipwa kupitia Mifuko hii kwa mujibu wa Sheria ambayo tumeipitisha mwaka jana. Nataka niseme kwamba, tunalipa kwa miezi sita, Watumishi wengi hawaelewi kwamba tunatakiwa kulipa mwezi wa Januari na Julai na tunatakiwa kulipa baada tu ya kumaliza malipo ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, mishahara tunaanza kulipa kuanzia tarehe 23 mpaka 27, kuanzia tarehe 28 mpaka tarehe 30 ndiyo tunatakiwa kuingiza pensheni katika akaunti zao. Kama wapo Watumishi ambao bado wanachelewa kupata pensheni zao, naomba Mheshimiwa Mbunge tuonane ili tuweze kusawazisha hali hiyo.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watumishi wengi hasa wa Serikali malipo yao ni madogo mno ambayo hayafikii hata kima cha chini cha mshahara; je, Serikali ina utaratibu gani sasa hivi kuhakikisha kwamba wanawaongezea angalau kufikia kima cha chini cha mshahara ili kuweza kukidhi angalau kujikimu katika maisha yao kuliko ilivyo leo hii? Serikali inawasaidiaje na iwe inaongeza hivyo kwa maana ya kima cha chini kiwe ndiyo cha kuweza kuwalipa wale ambao kwa hivi sasa wanalipwa kidogo mno?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali zuri sana. Nataka niseme tu kwamba, nia ya Serikali ni kuwasaidia Wastaafu wake kila hali itakavyoruhusu. Sisi sote ni mashahidi, mwaka jana tu tulikuwa tunazungumzia pensheni kima cha chini ilikuwa ni shilingi elfu ishirini na moja, Bunge lako Tukufu limekubali na limeridhia kupitisha shilingi elfu hamsini, shilingi elfu hamsini ni kama asilimia hamsini ya kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, kila hali itakaporuhusu, nia ya Serikali ni kuongeza pensheni na mambo yakiwa mazuri basi hicho kima cha chini tunaweza tukakifikia siku za baadaye.

Na. 5

**Utekelezaji wa Miradi ya Umeme Makete**

**MHE. DKT. RAPHAEL B. MWALYOSI (K.n.y. MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia TANESCO ilipanga na kutenga fedha kwa ajili ya usambazaji wa umeme katika Vijiji vya Mfumbi, Matamba, Ujuni na Mpangala Wilayani Makete kuanzia Januari 2009:-

(a) Je, utekelezaji wa miradi hiyo umefikia hatua gani hadi sasa?

(b) Je, ni miradi mingapi ya usambazaji umeme vijijini inatekelezwa na Wakala wa Umeme (REA) Wilayani Makete?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miradi iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ipo katika Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini. Katika Wilaya ya Makete unatekelezwa na TANESCO. Gharama za kupeleka umeme katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge ni shilingi milioni 236. Utekelezaji wa miradi hiyo ambayo itapata umeme kutoka kwenye Gridi ya Taifa upo katika hatua zifuatazo:-

Mradi wa kusambaza umeme katika Kijiji cha Mfumbi unajumuisha ufungaji wa transfoma yenye uwezo wa KVA 100 na ujenzi wa kilomita mbili za njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 0.4, nguzo zimesambazwa eneo husika tayari kwa kuanza ujenzi.

Mradi wa Umeme wa Kijiji cha Matamba unajumuisha ufungaji wa transfoma yenye KVA 100 na ujenzi wa kilomita moja ya njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 na kilomita mbili za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4. Kazi za ujenzi zinatarajia kuanza baada ya kukamilika kwa taratibu za maandalizi.

Mradi wa Umeme Kijiji cha Ujuni unahusisha ufungaji wa transfoma ya uwezo wa KVA 50 na ujenzi wa kilomita moja ya njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4, nguzo zimeshafikishwa eneo husika na ujenzi unaendelea.

Mradi wa Umeme Kijiji cha Mpangala unahusisha ufungaji wa transfoma yenye ukubwa wa KVA 100 na ujenzi wa kilomita moja ya njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 na ujenzi wa kilomita 2.1 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4, nguzo zimeshafikishwa katika eneo la mradi na ujenzi wa mradi utaanza wakati wowote kuanzia sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wilaya ya Makete, hakuna Mradi wa Usambazaji umeme vijijini unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Hii inatokana na ukomo wa bajeti ya Mfuko kuhudumia maeneo mengi kwa pamoja. Hata hivyo, Serikali inafanya jitihada za kuongeza Bajeti ya Mfuko na kuwasiliana na

washirika wa maendeleo watakaochangia Mfuko huo ili uweze kuhudumia maeneo mengi zaidi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa katika Wilaya jirani na Makete (Wilaya ya Ludewa) kumekuwa na ahadi tangu 2006 kwamba tutapatiwa umeme kupitia Gridi ya Taifa kutokea Madapu na Mbunge wao amekuwa akiwaahidi wananchi utakuja na huu mwaka wa mwisho wananchi wanasema Profesa Mwalyosi mwongo; nataka Mheshimiwa Waziri aseme hapa anawaambiaje Wananchi wa Ludewa kuhusu kupatikana umeme wa Gridi ya Taifa Ludewa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hapo hali ni tete kidogo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimtoe wasiwasi tu kwa sababu Wilaya ya Ludewa imepatiwa majenereta mawili ambayo bahati nzuri wakati wa ufunguzi wa huduma hiyo pale Ludewa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, alikwenda mwenyewe akafungua. Suala la kupatiwa umeme wa gridi Ludewa linatokana na kukamilika kwa Mradi wa Makambako – Songea, ambao utatoa umeme Makambako kwenda Songea na kuingia Madata kwenda Mbinga na matarajio ni kufika mpaka Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi kwa sababu huo Mradi wa Makambako - Songea haujamalizika, napenda nimhakikishie Mbunge na ninasema hili ili wapiga kura wasikubane; ahadi hiyo inaendelea kutekelezwa na bado Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Sweden, ambayo itatupa karibu dola milioni sabini kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Makambako - Songea ambao ndiyo utapeleka umeme wa gridi.

Kwa hivi sasa tukubaliane tu kwamba, majenereta mawili yaliyofika pale yanakidhi sana mahitaji ya Ludewa Mjini, lakini bado Mradi huo wa Gridi unaendelea kutekelezwa.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa takriban leo miaka hamsini toka nchi yetu imepata uhuru vijiji vingi bado havijapata umeme; je, nini maoteo ya Wizara kuhakikisha kwamba vijiji vyote vitakuwa vimepata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Arfi kwamba, miaka hamsini iliyopita upatikanaji wa umeme kwa Tanzania ulikuwa katika maeneo machache sana na katika miaka hamsini hii

Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kusambaza umeme mijini na pia kwenye maeneo mengi vijijini.

Mheshimiwa Spika, Watanzania asilimia kumi na nne wanapata umeme ambao ni asilimia ndogo lakini bado inatarajiwa kwamba katika miaka mitatu, minne, inayokuja tutafikisha upatikanaji wa umeme kwa Watanzania asilimia 20 na 25, lakini nchi yetu ni kubwa na idadi ya Watanzania sasa hivi inafikia milioni arobaini.

Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata nchi ambazo zina uwezo mkubwa sana kiuchumi kama Afrika Kusini, bado wanafikisha umeme kwa watu asilimia 45 na 50. Kwa hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaendelea na utekelezaji wa mipango ili kuhakikisha kwamba, Watanzania wengi zaidi wanapata umeme.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa usambazaji wa umeme huu wa TANESCO unafanana na ule wa Mnazi Bay; na kwa kuwa tayari kazi ya kusambaza nguzo na nyaya za umeme kutoka Nyangao kwenda Ndanda umeanza; je, Serikali inaweza kutuhakikishia hapa kwamba watamalizia kusambaza nguzo, nyaya na kuwasha umeme kama ilivyopangwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Kumchaya kwamba, kazi ya kupeleka umeme kutoka Nyangao mpaka Ndanda itakamilika mwezi Februari 2010, kwa maana ndani ya wiki mbili au tatu kazi hii itakamilika na ni matarajio yetu kwamba *commissioning* itaanza na Wakazi wa Masasi watapata umeme wa gesi kutokea chanzo cha Mnazi Bay ambao una uhakika zaidi. Kwa hiyo, matatizo yanayotokana na jenereta Masasi yataondoka.

Naomba nikuahidi kwamba, wakati wa *commissioning* hiyo, Waziri wa Nishati na Madini ameniahidi kwamba ama yeye au mimi, tutakwenda kushuhudia ufunguzi huo ndani ya wiki mbili au tatu. (*Makofi*)

Na. 6

**Upungufu wa Nishati ya Umeme Nchini**

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Kwa kuwa upungufu wa nishati nchini umekuwa ukiitatiza Serikali kwa muda mrefu sasa; na kwa kuwa utafiti uliofanyika mwaka 2007 *(household survey)* unaonesha kuwa wananchi waliounganishwa kwenye Gridi ya Taifa wameongezeka kwa asilimia 10 (2001) hadi asilimia 12 (2007); na katika ongezeko hilo maeneo yaliyo nje ya Jiji la Dar

es Salaam na ya Vijijini yaliyounganishwa ni asilimia 2.5 (mwaka 2007) jambo linalofanya maeneo mengi kubaki katika hali mbaya sana:-

(a) Je, kuna ongezeko la asilimia ngapi kuanzia mwaka 2007 hadi 2010?

(b) Je, ni kwa kiasi gani ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa mwaka 2005 kuondoa tatizo la umeme imetekelezeka?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, asilimia 14 ya Watanzania wanatumia nishati ya umeme, ambapo asilimia 12 ni watumiaji wa mijini na asilimia mbili ni watumiaji wa vijijini, hivyo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2007 ambapo asilimia 10 ya Watanzania walikuwa wanapata umeme hadi 2010 kuna ongezeko la asilimia 4.0.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mipango ya muda mfupi, wa kati na mrefu wa kuboresha huduma za makusudi za kiusimamizi zikiwemo mpango wa miaka mitano wa kuimarisha hali ya kifedha ya TANESCO uliopitishwa na Serikali mwaka 2006; Mpango wa Dharura wa Kuongezeka Kiwango cha Uzalishaji wa Umeme *(Emergency Power Program*) ulioidhinishwa na Serikali mwaka 2006; na Mkakati wa Kurekebisha Sekta ya Umeme *(Power Sector Reform Strategy)* umetayarishwa na uko kwenye mchakato wa kupata ridhaa ya Serikali.

Hatua nyingine ni uanzishwaji wa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) na Mfuko wa Nishati Vijijini (*REF)* ulioanza kazi mwaka 2007, Sheria mpya ya Umeme iliyopitishwa na Bunge na kuridhiwa na Rais mwaka 2008; na Mdhibiti wa Sekta ya Nishati (EWURA) aliyeanza kazi mwaka 2006 na Mpango Kamambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme *(Power System Master Plan - PSMP*) uliokamilishwa mwaka 2008 na kupitishwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kwa pamoja, Mipango na Mikakati hiyo ilifanikisha ujenzi wa mitambo ya kudumu inayotumia gesi ya jumla ya MW 140; TANESCO ilikopeshwa shilingi bilioni 300 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini; Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kununua majenereta mapya 17 kwa ajili ya Kigoma Mjini, Kasulu, Kibondo, Sumbawanga, Nkasi na Ngorongoro - Loliondo.

Aidha, Makao Makuu ya Wilaya ya Ukerewe, Serengeti, Mbinga, Simanjiro, Mkinga na Kilolo, zimepatiwa umeme; Makao Makuu ya Wilaya za Bahi na Uyui zitapata umeme kufikia mwisho wa Februari 2010 kwa ufadhili wa Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini. Makao Makuu ya Wilaya za Nanyumbu na Bukombe zilizobaki zipo katika programu ya kupatiwa umeme kwa ufadhili wa Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na washirika wetu wa maendeleo inakamilisha taratibu za kifedha kwa ujenzi wa njia kuu ya usafirishaji umeme Iringa - Dodoma, Singida - Shinyanga ya msongo wa Kv 400 ili kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, hivi sasa mchakato wa kukamilisha ununuzi wa majenereta ya MW 60 kwa ajili ya Kanda ya Ziwa na MW100 kwa Dar es Salaam unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea pia kuweka mazingira mazuri kuwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuendeleza Sekta ya Umeme hususan katika nyanja ya uzalishaji wa umeme na usambazaji.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, bado asilimia kumi na nne ni ndogo sana hasa ukizingatia Watanzania ni milioni arobaini kwa hiyo ina maana asilimia kumi na nne ya Watanzania ni kama watu milioni tano tu wanaopata umeme Tanzania hasa ukizingatia kwamba sasa hivi teknolojia nyingi zinahitaji umeme; je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kuhakikisha kwamba walau Watanzania zaidi ya 25 wanapata umeme ifikapo mwaka 2015?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nimesema katika jibu la msingi kwamba katika miaka miwili, mitatu iliyopita, tumetoka asilimia kumi hadi asilimia 14. Kweli bado ni asilimia ndogo, lakini kama nilivyosema uwekezaji ndani ya Sekta ya Umeme una maeneo matatu; una eneo la uzalishaji, una eneo la usafirishaji na una eneo la usambazaji. Swali lako limejikita katika eneo la usambazaji.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Tanzania wengi bado kwenye maeneo ya vijijini asilimia sabini, kwa hiyo tunaposema kuwafikishia umeme maana yake kuna jambo la uzalishaji lakini pia jambo la usafirishaji na wakishafikiwa hapo ndiyo linakuja suala la usambazaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema Serikali inaendelea kwenye uwekezaji kwa maeneo matatu yote haya ili kuhakikisha kwamba Watanzania walio wengi, wananufaika zaidi na huduma hii ambayo sasa si anasa lakini ni sehemu ya mikakati ya maendeleo na mipango ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Suzan Lyimo kwamba, mipango hiyo imo kwenye *Power System Master Plan* na mipango mingine ambayo tumewasilisha ndani ya Bunge lako hili Tukufu.

Na. 7

**Mikopo kwa Wanafunzi Wanaotakiwa Kujiunga na Vyuo Vikuu**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ya Juu kwa Taifa lolote inalenga kuwaandaa wataalam mbalimbali kuja kukabiliana na majukumu mazito katika jamii; na kwa kuwa Serikali haitoi mikopo kwa wanafunzi wote walio na haki ya kujiunga na Vyuo Vikuu:-

(a) Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba umefika wakati kufanya juhudi zinazowezekana ili wanafunzi wote wanaoingia Vyuo Vikuu wapatiwe mikopo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutowapatia mikopo wanafunzi wote kunawafanya baadhi ya wanafunzi kutokupata muda wa kutosha kushughulikia masomo bali kutafuta fedha za ada na matumizi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Elimu ya Juu ni muhimu kwa Taifa lolote kwa kuwa inaandaa wataalam wa fani mbalimbali kulingana na mahitaji ya maendeleo ya jamii husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingependa kugharamia wanafunzi wote wenye sifa za kujiunga na Elimu ya Juu; hata hivyo kutokana na uwezo mdogo wa kiuchumi, haina uwezo wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wote. Serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wasio na uwezo kiuchumi wanapatiwa mikopo. Aidha, Serikali imekuwa inaongeza fedha za mikopo ya wanafunzi kama ifuatavyo:-

Mwaka 2005/06 idadi ya wanafunzi 42,729 kiasi cha fedha kilichotolewa 56.2 bilioni; mwaka 2006/07 wanafunzi 47,554 Shilingi 76.2 bilioni zilitolewa; mwaka 20087/08 wanafunzi 55,687 shilingi 112.5 bilioni zilitolewa; mwaka 2008/09 wanafunzi 58,841 shilingi 140.3 bilioni zilitolewa; na mwaka 2009/10 wanafunzi 69,442 shilingi 197 bilioni zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imefanya juhudi kubwa sana kuhusiana na suala la mikopo ya wanafunzi. Hadi sasa inaongoza kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi wa elimu ya juu katika Afrika Mashariki. Hata hivyo, Serikali inatoa wito kwa Watanzania wenye uwezo kiuchumi kuchangia gharama za Elimu ya Juu kwa kuwalipia watoto wanaowalea ili fedha zilizopo zitumike kuwapa mikopo wale wenye mahitaji. Sera ya Uchangiaji ni kwa maendeleo ya Taifa kwani hutoa fursa zaidi kwa Watanzania kujiunga na Elimu ya Juu.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa wanaosumbuka sana na mikopo ya Elimu ya Juu ni watoto wa watu maskini na ikiwa inafahamu; ina mpango gani wa kuwasaidia watoto hawa ili na wao waweze kusoma wakiwa wametulia na siyo kuombaomba na kupiga simu kwa watu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, tumekiri kwamba, mikopo hii ni kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji wakiwemo watoto maskini, lakini pia watoto waliofaulu wa Kitanzania na vigezo vingine ambavyo tunafikiri ni muhimu kuvitumia kutoa pesa hiyo kidogo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tulichosema ni kwamba hatuwezi kutoa pesa kwa Watanzania wote kwa sababu pamoja na kwamba Serikali ingependa ifanye hivyo, haina pesa ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba wanafunzi hawa hawana sababu ya kupoteza masomo kwenda kufuatilia mikopo Bodi ya Mikopo, utaratibu ni wazi na wanafunzi hawa wanajaza fomu wakiwa mashuleni, fomu zile zinatakiwa zitumwe kwa wakati Bodi ya Mikopo na zinashughulikiwa kwa wakati na mikopo inapelekwa katika vyuo vyao. Kwa hiyo, hawana sababu ya kupoteza muda kwenda kufuatilia mikopo Bodi ya Mikopo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED**: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Rais aliwaahidi Watanzania kwamba hakuna mtoto yeyote wa Kitanzania maskini ambaye anaweza kusoma asiweze kupatiwa elimu; Watanzania wengi kwa kuelewa uwezo wa Serikali yetu wamejitahidi kuwasomesha watoto wao, lakini wamefika pahala wazazi hao wamekwama; je, Serikali inasema nini katika kutekeleza ile Ahadi ya Rais kwamba hakuna Mtanzania yeyote atakayekosa elimu kwa sababu ya uwezo wa kifedha wakati wazazi wameshachangia kiasi fulani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tunachangia elimu ya wanafunzi kutoka primary, sekondari na pia Elimu ya Juu kwa kuwapa mikopo, lakini tukumbuke kwamba, Elimu ya Juu maana yake wanafunzi, wazazi au walezi wachangie.

Mheshimiwa Spika, Ahadi ya Rais iko pale pale na tunawapa wanafunzi mikopo lakini tukumbuke kwamba kuna vigezo zaidi ya hali hiyo ya umaskini. Kwa hiyo, lazima kwanza wanafunzi hao wafaulu na wewe ukiwa maskini unaagalia priority yako ni nani, ni wale waliofaulu na ni nani ambao watakusaidia kuondoa umaskini kwa haraka zaidi katika nchi maskini kama hii. Kwa hiyo, hivyo ndiyo vigezo tulivyoviweka na hii yote inasaidia katika kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji na kuwapa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Ahadi ya Rais iko pale pale, inategemea kila aliyeisikia ameitafsiri vipi, lakini hali halisi ndiyo hiyo Serikali inasomesha wanafunzi kutoka Elimu ya Awali mpaka Elimu ya Juu lakini elimu ya juu ni lazima wananchi wachangie.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Utoaji wa mikopo wa Elimu ya Juu, unategemea vigezo ambavyo vimewekwa; na kwa maana ya Ahadi ya Mheshimiwa Rais, wanafunzi ambao wanastahili kupewa mikopo ni wale waliopata division one na division two katika mitihani ya kidato cha sita au wale wanaochukua sayansi au wale ambao wanachukua ualimu katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa wanafunzi wote ambao wametimiza vigezo hivyo wamepewa mikopo na Serikali. Aidha, kuna uvumi unaosema kwamba, kuna ukomo katika kutoa mikopo katika Elimu ya Juu, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali haikuweka ukomo katika kutoa mikopo ya Elimu ya Juu na wanafunzi wote ambao wametimiza vigezo vya kupewa mkopo watapewa mkopo huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa uthibitisho huo.

Na. 8

**Uhakiki wa Madeni ya Walimu**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS (K.n.y. MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilisema imeshahakiki madeni ya walimu na mchakatowa malipo hayo utaanza haraka iwezekanavyo:-

(a) Je, hadi sasa walimu wangapi wameshalipwa na wangapi hawajalipwa kwa mchanganuo wa kila mkoa?

(b) Kwa kuwa kumejitokeza malalamiko kwa baadhi ya walimu kulipwa fedha pungufu ya madai yao katika mikoa mbalimbali kwa wale waliobahatika kulipwa; je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuwapatia fedha zilizosalia haraka bila kikwazo chochote?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa ninakuomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye rehema kwa kuniwezesha kuvuka salama na kunifikisha hapa. Namwomba anifanyie wepesi katika majukumu aliyonijalia. Amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa uhakiki wa madeni ya walimu wa shule za msingi ulikamilika mwezi Februari 2009 na madeni ya walimu wa sekondari, vyuo vya ualimu na wakaguzi wa shule ulikamilika mwezi Oktoba mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki, jumla ya walimu 61,423 walilipwa. Walimu waliolipwa ni wale ambao madai yao yalikidhi sheria, taratibu na kanuni za fedha za umma na yalilipwa kupitia Halmashauri katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, jumla ya madai ya walimu 14,215 yalikataliwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutofuata taratibu, kughushi nyaraka, kuwasilisha madai yaliyokwishalipwa na madai kutokuwa na vielelezo au nyaraka zinazojitosheleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatoa agizo kuwa wale walimu ambao hawakulipwa kabisa au hawakubaliani na kiasi walicholipwa au wale ambao wanazo nyaraka za kuthibitisha madai yao, wawasilishe malalamiko yao kwa Wakurugenzi wa Halmashauri husika ili madai yao yapatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, orodha ya mikoa yote 21 ya Tanzania Bara ni ndefu, naomba tuiwasilishe kwa mhusika. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Pengine itapendeza Waheshimiwa Wabunge wote wapate nakala.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bado kuna mkanganyiko mkubwa juu ya suala zima la malipo ya walimu:-

(a) Pamoja na juhudi za Serikali zinazochukuliwa kuliondoa tatizo hilo kwa nini basi Wizara/Halmashauri za Mikoa hazimwandikii mwalimu mmoja sababu zilizomfanya asilipe badala ya kutoa sababu za jumla kitu ambacho mwalimu hajui vipi ajitetee?

(b) Kwa kuwa bado mchakato huu haujamalizika ingawa Mheshimiwa amesema umemalizika; je, ni lini sasa mchakato huu utamalizika rasmi ili kuondoa tishio la mara kwa mara la Chama cha Walimu Tanzania la kuitisha migomo hasa ukitilia maanani kwamba kuna walimu 14,215 bado hawajalipwa kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri na hasa kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi na suala hili linaweza kuwa ni fimbo mojawapo la kuisulubu CCM 2010? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, walimu ni sehemu ya watumishi wa umma, wanaongozwa na wanatawaliwa kwa Sheria za Utumishi wa Umma. Madai haya yalikusanywa na Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, yakakabidhiwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Amekagua akajiridhisha akatoa kibali kuwa idadi ile ilipwe. Hatujafunga milango, tumesema wale ambao hawajaridhika ama wanao ushahidi wapeleke, haki yao kama ipo itapatikana.

Mheshimiwa Spika, mchakato katika utumishi hauwezi kuisha na ndio maana tumesema na Mheshimiwa Celina Kombani ameagiza kusitokee tena malimbikizo. Watalipwa tu, lakini hakuna tishio la Chama cha Walimu kukisulubu Chama cha Mapinduzi; tuko imara yao, ni haki yao na Watumishi wote wa Serikali wanaodai Serikali ni haki yao kupeleka madai yao watalipwa na CCM itashinda. (*Makofi*)

Na. 9

**Ujenzi wa Barabara ya Lami Korogwe – Handeni**

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika barabara inazozijenga kwa kiwango cha lami ni pamoja na ile ya Korogwe – Handeni:-

(a) Je, ujenzi wa barabara hiyo umefikia wapi?

(b) Kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu kiusalama na kiuchumi katika kuunganisha Mikoa ya Magharibi, Kati na Bandari ya Tanga; je, ni lini Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kiteto –Kongwa itajengwa kwa kiwango cha lami?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mkataba wa ujenzi wa barabara ya Korogwe hadi Handeni yenye urefu wa kilomita (65) kwa kiwango cha lami, ulisainiwa tarehe 15 Juni, 2009. Kwa sasa Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya Sinohydo kutoka China, anaendelea na kazi ya kujenga kambi, kuleta mitambo na wataalam kwenye eneo la mradi, tayari kwa kuanza kazi ya ujenzi wa barabara hii. Ni matarajio yetu kuwa, kazi ya ujenzi wa barabara itaanza rasmi ifikapo mwezi Mei 2010.

Kazi ya uthamini wa nyumba, mazao na mali nyingine zitakazoathiriwa na ujenzi wa barabara hii pia umekamilika. Kulingana na uthamini uliofanyika, gharama za fidia zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.1. Wananchi walioathirika watalipwa fidia zao kulingana na taratibu zilizopo ili kupisha ujenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii inayounganisha Bandari ya Tanga na Mikoa ya Kati na Magharibi, Serikali imeanza mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu kwa barabara ya Handeni – Kibirashi – Kibaya – Chemba hadi Singida yenye urefu wa km. 433. Taratibu za manunuzi zipo katika hatua za mwisho na inatarajiwa kuwa, Mkataba wa Upembuzi yakinifu utasainiwa mwezi Machi 2010. Aidha, sehemu ya barabara kutoka Kibaya – Dosidosi hadi Kongwa itafanyiwa mchakato kwa kadiri fedha zitakavyopatikana.

Na. 10

**Umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi Mjini**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Moshi ndio Mji wa Mlima Kilimanjaro ambao ndio unaongoza kwa kuingiza pata kubwa la utalii; na kwa kuwa TANAPA/KINAPA ina mpango maalum wa kukarabati njia zote zinazotumiwa na watalii kupanda Mlima Kilimanjaro:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi Mjini katika kukuza utalii?

(b) Je, Serikali itakubali ombi la Wakazi wa Moshi Mjini kuwa kiwanja hicho kihusishwe katika ukarabati kwani ni moja ya njia wanayotumia watalii?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi katika kuhudumia wasafiri hususan watalii wanaotumia kiwanja hiki. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali ilikusanya mapato ya shilingi 4,361,492 kutokana na ndege zinazotumia kiwanja hiki. Hata hivyo, Serikali ilitumia shilingi 88,161,603 kukifanyia matengenezo kiwanja hiki, yaliyowezesha ndege kuruka na kutua salama. Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010 inatarajia kukusanya shilingi 4,400,000 kutokana na matumizi ya kiwanja hiki, wakati huo huo inatarajia kutumia shilingi 185,900,000 kukifanyia matengenezo ya kawaida ili kuwezesha ndege zinazotumia kiwanja hiki kuruka na kutua salama. Hivyo ni dhahiri kuwa Serikali inatambua umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi Mjini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukifanyia matengenezo Kiwanja cha Moshi ili kuwezesha ndege zinazotumia kiwanja hiki kuruka na kutua salama wakati jitihada za kutafuta fedha za kukifanyia ukarabati unaostahili zikiendelea. Aidha, Serikali haina kipingamizi katika kujumuisha ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi katika

programu ya ukarabati wa njia zote za utalii chini ya TANAPA/KINAPA. Ili kufanikisha mpango huu, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itawasiliana na TANAPA/KINAPA kwa ajili ya kufanikisha Mpango huu.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri hayakuniridhisha sana kwa sababu fedha zinazosemwa zimetumika (shilingi milioni 84) ni fedha nyingi sana lakini mpaka sasa Precision haiwezi kutumia kiwanja kile kwa sababu mashimo yaliyoko katika kiwanja kile ni makubwa na hakuna commercial plane yoyote inayotua katika Kiwanja cha Moshi kwa zaidi ya miaka mitano sasa. Kwa hiyo, labda Waziri angetuambia ni matengenezo gani yametumia fedha nyingi namna hiyo?

La pili ni litakuwa ombi; kwa sababu Wizara ya Utalii ndiyo hasa inayohusika katika kutumia kiwanja hiki, tungeomba Wizara ikabidhi kiwanja hiki KINAPA ili iweze kukihudumia vizuri kiweze kutumika kwa ajili ya watalii.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya fedha makubwa ambayo bado hayajawezesha ndege kubwa kutua katika kiwanja hicho; fedha hizi kweli ni nyingi, kwa miaka miwili iliyopita Kiwanja cha Ndege cha Moshi tulikitengea fedha na kufanya matumizi katika kiwanja hicho jumla ya shilingi milioni 288, lakini kwa kulinganisha na kile cha Shinyanga tulitenga fedha jumla ya shilingi milioni 397. Bado matumizi ya kiwanja hicho au uhitaji wa matumizi ya kiwanja hicho hayafanani na maeneo mengine, kwa mfano, tumetumia fedha kama hizo idadi ya abiria kwa Moshi walikuwa 713 kwa mwaka 2008/2009 kule Shinyanga ilikuwa 13,000. Kwa hiyo, pamoja na kwamba imetumika hela nyingi, kiwanja hiki kimetumiwa zaidi na watalii kuliko watu wengine. Tutaendelea kutenga fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kukipanua kama tulivyofanya Kiwanja cha Arusha ili kiwezeshe ndege kubwa zaidi ziweze kutua katika kiwanja hicho.

Swali la pili la kukabidhisha kiwanja hiki kwa KINAPA, wala hakuna umuhimu mkubwa wa kufanya hivyo kwa sababu ya kuwahudumia watalii. Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu imetenga fedha za kutosha na imekifanyia matengenezo makubwa Kiwanja cha Ndege cha Arusha na wala siyo KIA, ambacho sasa kinahudumia abiria wengi zaidi na kinatoa huduma kubwa sana kwa watalii kushinda kiwanja kingine chochote hapa Tanzania. Tutafanya hivyo hivyo kuhakikisha kwamba Kiwanja hiki cha Moshi nacho kinakuwa katika hali nzuri.

**MHE. ALYOCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ni kweli kwamba kiwanja hicho kina mashimo ambayo hayawezeshi ndege kubwa kutua. Vilevile kiwanja hicho kimevamiwa na wananchi ambao wameanza kujenga nyumba za kudumu kwenye maeneo ya kiwanja hicho; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia hapa kwamba atatoa pesa za kujenga fensi eneo la kiwanja hicho ili wananchi wasiendelee kuvamia? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba niseme kwamba ni kosa kubwa kuvamia eneo la viwanja vya ndege; imetokea katika mikoa mingi na katika viwanja vingi. Hili tatizo ni kubwa kwa sababu tutachukua hatua za kisheria kwa wananchi ambao wanavamia viwanja hivyo ambavyo vitaleta athari kwa wananchi hao.

Ningetoa mwito kwa wananchi wote kwamba, wale wote ambao wako maeneo ya jirani na viwanja waache tabia hiyo ya kuvamia. Upande wa Serikali tumeweka Mpango Mkakati madhubuti wa kutenga pesa kwa ajili ya kujenga uzio katika viwanja vyote Tanzania. Tumeanza utaratibu huo katika baadhi ya viwanja na Mpanda tunaanza hivi karibuni na katika viwanja mbalimbali ambavyo navyo vimeathiriwa na uvamizi. Kazi hiyo tutajitahidi kuifanya kwa kadiri pesa zitakavyopatikana na tunajaribu kuifanya mapema iwezekanavyo ili tuondoe adha hii ya viwanja vyetu kuvamiwa na wananchi kwa ujenzi wa makazi.

Na. 11

**Mpango wa Bima ya Afya ya Jamii**

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha Bima ya Afya ya Jamii ambapo kila familia inatakiwa kutoa shilingi elfu kumi ili ipate matibabu na dawa bure kwa mwaka mzima kwenye Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya:-

(a) Je, Serikali ina taarifa kuwa mpango bado haujaeleweka kabisa kwa wananchi wengi?

(b) Je, Serikali inafanya mkakati gani wa kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuhusiana na mpango huu?

(c) Kwa kuwa zahanati na vituo vingi vya afya huwa havina madawa; je, Serikali haioni kuwa wanaumia kwa kuchangia bima hii kisha wanaandikiwa wakanunue dawa kwenye maduka binafsi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Afya ya Jamii *(Community Health Fund - CHF),* unalenga hasa kutoa huduma za aina ya Bima kwa Watanzania wengi wanaoishi vijijini. Michango inayotolewa na wananchi ni kwa kiwango ambacho wanachama wa Halmashauri husika wamekubaliana, hivyo kiwango kinatofautiana toka Halmashauri moja hadi nyingine.

Serikali imebuni mpango wa tele kwa tele kwa nia ya kufuatilia michango toka kwa wanachama. Katika mpango huu, Serikali Kuu inatoa kwa Halmashauri kiasi cha fedha sawa na kile kinachokusanywa na Halmashauri.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Mpango huu wa Mfuko wa Afya ya Jamii ulianza kwa majaribio katika Wilaya chache, baada ya kuonesha mafanikio katika wilaya hizo hatua iliyofuata ni kuziwesha Halmashauri zote kuanzisha mfuko huu. Ingawa maudhui ya Mfuko huu hayajaeleweka vizuri kwa watu wote, idadi ya wananchi ambao wanauelewa inaongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na uraghibishi na elimu inayotolewa.

(b) Katika hatua za awali za uanzishaji wa Mfuko huu, Wizara ilijikita zaidi katika kuziwezesha Halmashauri kuunda vyombo vya usimamizi kwa huduma za afya, yaani Bodi na Kamati za Afya, ambazo hadi sasa tayari zimeshaundwa katika kila Halmashauri. Ni matarijio ya Wizara kwamba, kwa kupitia Bodi na Kamati za Afya za Halmashauri, wananchi wataweza kufahamishwa na kuhamasishwa zaidi kuhusiana na umuhimu wa Mfuko.

(c) Jukumu la kuvipatia dawa na vifaa tiba vituo vya afya na zahanati ni la Serikali Kuu. Madhumuni ya Mfuko wa Afya ya Jamii ni kuziwezesha Halmashauri kuwa na pesa karibu ambazo zinaweza kutumika kukidhi dharura kama vile kuishiwa dawa muhimu, mahitaji ambayo hayakutarajiwa na hayako katika bajeti au kufanya ukarabati na matengenezo madogo madogo ya vituo vya kutolea huduma. Pesa za Mfuko haziwezi kukidhi mahitaji yote ya dawa. Katika kushughulikia changamoto ya upatikanaji wa dawa, Serikali kwa upande wake imekuwa ikijitahidi kuongeza bajeti ya dawa mwaka hadi mwaka.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kubuni na kuanzisha bima hii ya afya ya jamii na wananchi wameipokea kwa mikono miwili jimboni kwangu, wameishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ambalo linakera kwenye utaratibu huu, mwananchi anapochangia anapolipa kiasi kinachotakiwa anaamini kwamba sasa atakwenda zahanati, atakwenda hospitali ataandikiwa dawa na atapata lakini tatizo anaandikiwa anakwenda kumwona Daktari anaandikiwa dawa anaambiwa akanunue. Sasa mara nyingi wananchi wanakata tamaa na idadi ya wale ambao wanajiandikisha inapungua kwa sababu hiyo.

Je, Serikali itafanya utaratibu ili wale wanaondikiwa kununua dawa hatimaye warudishiwe fedha ambazo wananunulia dawa? Serikali itakubali kuanzisha utaratibu huo ili wananchi wengi zaidi waendelee kujiunga?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru sana kwa pongezi zake alizotoa kwa Serikali. Ni kweli kabisa kwamba saa nyingine unakuta wataalam wakiandika dawa wanawaandikia na kuwaambia waendee wakanunue kama dawa hazipatikani. Tatizo kubwa ambalo mimi naliona ni kwamba tumetoa orodha ya dawa muhimu katika zahanati zote na vituo vyote vya Serikali ambazo zinatakiwa zipatikane pale.

Mara nyingi unakuta watu wanaandika dawa ambazo haziko katika orodha ya dawa zile muhimu. Sasa nachotaka kusema kwa sababu Mfuko wa Afya unasaidia kununua dawa ambazo zinakosekana wakati MSD wakiwa wanaleta dawa, ningependa tu nitoe ushauri kwamba, madaktari ambao wanawaona wagonjwa wawaandikie dawa ambazo ziko katika orodha ambayo inapatikana katika hospitali badala ya kuandika dawa ambazo hazipo pale na kuwatuma waende kununua madukani.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kwa sasa hivi hakuna utaratibu wa kurudisha zile dawa ila ni kuwasisitiza kwamba waandike dawa ambazo zinapatikana na watumie dawa na pesa kununulia dawa na sisi kama Serikali tunaongeza bajeti ya dawa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mfuko huu wa Bima ya Afya umeendelea kuwasaidia sana wananchi kwani katika familia kwa wastani mtu anatibiwa kwa fedha isiyozidi shilingi 2000 kwa mwaka lakini kwenye hizi shule zetu za sekondari na vyuo mwanafunzi mmoja analazimika kulipa fedha sio chini ya shilingi 20,000 kwa mwaka kwa ajili ya matibabu. Ningependa kufahamu Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kwamba mpango kama huu wa Bima ya Afya unapelekwa mpaka mashuleni ili wanafunzi waweze kutibiwa kwa gharama nafuu zaidi kuliko 20,000 wanayolipa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, mwanafunzi anapokwenda shule kama atakuwa amechangia Mfuko wa Afya anahitajika atibiwe katika hospitali iliyoko katika eneo la shule. Lakini ni kweli kabisa tatizo hilo sisi tumeliona na ushauri ambao tumeutoa ni kwamba, shule inayokuwepo pale lazima iwasiliane na Halmashauri husika ili wanapotoa shilingi 10,000 katika shule husika wataweza kukubaliana kuona kwamba ni kiasi gani anatakiwa kulipa mwanafunzi na kiasi ambacho shule inaweza kukusanya. Baada ya kukusanya zile pesa wanazipeleka katika Halmashauri ili wale wanafunzi waweze kupata huduma kwenye zahanati au kituo cha kutolea huduma kilichopo karibu nao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii kuwakumbusha wataalam na wakuu wa shule katika maeneo ambayo wanaishi na watoto ambao wako katika sekondari au shule nyingine, wawasiliane na Halmashauri husika ili uwepo utaratibu wa kuweza kuhakikisha kwamba pesa kidogo ya wanafunzi inachukuliwa na kuweza kuchangia kwenye Halmashauri waweze kupatiwa dawa. Vilevile tutamuagiza Katibu Mkuu aweke utaratibu mzuri na kuwaeleza shule na Halmashauri tukishirikiana

na TAMISEMI, watoto hawa wanaweza kupata matibabu kwa bei nafuu kuliko ambavyo sasa hivi inatokea.

Na. 12

**Sera ya Afya Nchini**

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI (K.n.y. MHE. MAGDALENA H. SAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Afya Nchini inasema huduma za afya ni bure kwa akina mama wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wazee wenye umri zaidi ya miaka sitini wasiokuwa na uwezo; na kwa kuwa zaidi ya asilimia thelathini ya makundi hayo hawapati huduma hiyo bure:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza Watanzania fedha hizo zinazotengwa kila mwaka kwa njia ya makundi hayo zinakwenda kwenye Mfuko gani na zinafanya kazi gani?

(b) Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa maagizo mara kwa mara kwa Watendaji kutoa huduma hizo bure hospitalini; na kwa kuwa sehemu kubwa ya maagizo hayo hayatekelezwi; je, ni watendaji wangapi wamechukuliwa hatua za kinidhamu kwa kukiuka maagizo hayo ya Serikali na kusababisha adha kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kimsingi, Serikali haitengi fedha kwa ajili ya makundi ya misamaha peke yake. Watu katika makundi ya misahama wanapata huduma ya tiba pamoja na wananchi wengine katika vituo vya kutolea huduma za afya ambavyo vinapata fedha za kununulia dawa na vifaa kutoka Serikalini. Kwa maneno mengine, Bajeti ya Afya inalenga wananchi wote kwa ujumla wake na siyo kundi moja moja. Aidha, Serikali haina taarifa rasmi zinazothibitisha kwamba, zaidi ya asilimia 80 ya wananchi walio katika kundi la msamaha hawapati huduma bure kama ilivyonukuliwa na Mheshimiwa Mbunge.

(b) Ingawa hakuna takwimu sahihi za waliochukuliwa hatua za kinidhamu kila malalamiko yanayopotokea kuhusu kutopatikana huduma bila kulipia kwa makundi haya, hatua mahususi huchukuliwa na viongozi wa vituo husika pale ukiukwaji unapotokea. Mara nyingi malalamiko haya husababishwa na ukosefu wa dawa au vifaa tiba katika vituo hivyo; hali hii husababishwa na mambo mbalimbali yaliyo nje ya uwezo wa mtoa huduma. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote wakiwemo watu wa makundi maalum kwa kufanya yafuatayo: Kuboresha mfumo wa upatikanaji wa dawa na vifaa katika vituo; kuongeza idadi ya

watumishi katika vituo; na kuendelea kuwakumbusha watoa huduma kuzingatia maelekezo ya sera kwa makundi hayo.

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. nasikitisha kwamba Serikali haina taarifa rasmi ya kwamba akinamama wajawazito, watoto wengi ambao wako chini ya umri wa miaka mitano na wazee ambao hawana uwezo, hawapati huduma kama sera inavyosema lakini kufuatana na taarifa ya taasisi za utafiti na hata zile za Kamati yangu ya Huduma za Jamii ambayo inatembelea katika hospitali nyingi nchini, imebaini kwamba makundi haya maalum wengi wao hawapati huduma za afya bure katika hospitali.

Je, haijafika wakati sasa Serikali ifanye utafiti wake na iweke utaratibu mzuri zaidi ili makundi haya ya akinamama wajawazito, watoto ambao wako chini ya umri wa miaka mitano na wazee wasio na uwezo wapate huduma za afya bure na za kueleweka? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali la msingi sikusema kwamba Serikali haijui kwamba watoto au wajawazito ambao wanatakiwa wapate huduma bila malipo wengine wanakosa hizi huduma. Swali la msingi limeuliza takwimu na yeye alivyoniuliza ameniambia ni watu wangapi ambao naweza nikamtajia kwa takwimu kwamba wamekosa hizi huduma, lakini sikusema kwamba Serikali haifahamu.

Sasa yeye kama anazungumzia suala la kwamba Serikali hatujui kwamba wajawazito na watoto hawapati hizi huduma, hilo ni swali ambalo labda anataka nimpatie sasa hivi, lakini nilichosema ni kwamba muuliza swali alitaka kujua ni takwimu kiasi gani na yeye alisema asilimia themanini hawapati hizo huduma, ndio maana nikasema asilimia themanini kama anavyosema yeye, hatujaifanyia takwimu tukaona kwamba asilimia themanini ya yale makundi maalum yote hawapati huduma; ndio hicho nilichokanusha, lakini sikukanusha kwamba Serikali haijui. Naomba nieleweke hivyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho linaelekezwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali.

Na. 13

**Kilimo cha Mimea inayotoa Biofuel**

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na juhudi kubwa ya kupata mafuta kwenye mimea (*Biofuel*) na ardhi kubwa ya kilimo cha mazao ya chakula inatumika kwa ajili hiyo:-

(a) Je, umefanyika utafiti wa mafuta yatokanayo na nazi na kuona kama yanaweza kutumika kama nishati?

(b) Kama yanaweza kutumika hivyo kwa nini minazi ambayo inaweza kulimwa na mazao mengine isilimwe kwa wingi zaidi kuliko mibono na miwa ambayo hairuhusu kulimwa pamoja na mazao mengine?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri la Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mbunge Konde, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mafuta ya nazi yamefanyiwa utafiti katika maeneo mbalimbali duniani na hata hapa nchini na yameonekana yanafaa kutumika kama nishati mbadala wa mafuta aina ya dizeli.

(b) Mheshimiwa Spika, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) inayotekelezwa nchini, imekuwa inawahimiza wakulima kuandaa na kutekeleza Miradi ya Uendelezaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta kupitia DADPs. Mazao ya mbegu za mafuta yanayoendelezwa nchini ni pamoja na alizeti, ufuta, mawese, kartam na minazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuzalisha na kutumia mafuta ya nazi kama nishati mbadala, kikwazo kikubwa kilichopo kinahusu gharama kubwa ya uzalishaji wa mafuta hayo kutokana na ukweli kwamba, nazi nyingi hutumiwa kama sehemu ya chakula.

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Ingawa Mheshimiwa Naibu Waziri ameongelea kuhusu kuendeleza kilimo, lakini naona hakuna juhudi za makusudi za kuendeleza kilimo cha minazi katika nchi yetu. Chukulia eneo la Bagamoyo tu peke yake, kuna minazi mingi ambayo ni mizee na migonjwa; kwa nini hakuna juhudi za makusudi katika Ukanda wa Pwani ambao nazi zinaota kwa wingi za kuotesha minazi mingine mipya, yenye afya na kuongeza zao hili katika nchi yetu na hasa ukizingatia kwamba hata Bara sasa hivi minazi mingi inaota?

(b) Mheshimiwa Naibu Waziri ameongelea kuhusu gharama za kuzalisha mafuta kutoka kwenye nazi kwamba ni kubwa, lakini gharama hizo vile vile zinapatikana katika kutoa mafuta au kuzalisha mafuta kutokana na mibono na alizeti. Je, kuna tofauti gani sasa ya gharama za kuzalisha mafuta kutoka kwenye nazi na kuzalisha mafuta kutoka kwenye mazao mengine kama mibono na alizeti?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde kama ifuatavyo:-

Kwanza, nikiri kabisa kwamba Serikali imeweka juhudi kubwa kabisa kuendeleza zao la nazi na kama tunavyoelewa, tuna kituo chetu cha utafiti Mikocheni ambacho kinaendelea kufanya utafiti kwa magonjwa mbalimbali ya minazi, pamoja na kutoa miche bora ambayo ina ukinzani wa magonjwa na inayozaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama alivyosema, minazi mingi ni mizee; tunawashauri wakulima wa minazi kwamba minazi ikishafikisha takriban miaka hamsini, inatakiwa kung'olewa na kupandwa mingine na kwa sasa hivi minazi ambayo tunashauri wakulima wapande ni ile inayoitwa *East African Tall*, minazi yetu ya awali, ya tangu zamani, kwa sababu ndio yenye ukinzani na magonjwa.

Pia nawashauri Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo ya minazi kwamba, watumie DADPs, kwa ajili ya kuanzisha vikundi vidogovidogo ambavyo vitasaidia sana katika kuendeleza zao la minazi.

Mheshimiwa Spika, na kwa sasa hivi kama alivyotangaza Mheshimiwa Spika ni kwamba, Sheria yetu ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko imeshapita, nadhani bodi hii pia itasaidia katika kuendeleza zao la minazi hususan katika masula ya bei.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama za kuzalisha mafuta ya nazi ni kwamba, tofauti yake na mazao mengine, mazao mengine sijui lakini gharama ya kuzalisha lita moja ya mafuta ya nazi ambayo inaweza kutumika kama nishati ni shilingi elfu kumi na tano mia moja hamsini na moja na senti hamsini, ukilinganisha na shilingi elfu moja mia tano ya dizel. Kwa hiyo, moja kwa moja inaonekana kabisa kwamba, mafuta ya nazi haya itakuwa ni gharama kubwa kuyazalisha na kuacha dizel.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Kama kawaida matangazo; wageni waliopo Bungeni asubuhi ya leo ni wageni wa Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, ambao ni Ndugu Saley Jabri, naomba asimame; Ndugu Mohamed Jabri na Ndugu Abdallah Jabri. Vijana *smart* kabisa hawa, hatukuelezwa mahusiano yao na Mheshimiwa Anna Abdallah, lakini tunawakaribisha sana katika Ukumbi huu.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ni wajukuu zangu.

**SPIKA:** Aah, wajukuu eeh! Hawa ni wajukuu wa Mheshimiwa Anna Abdallah. Naomba Mwenyezi Mungu akuzidishie umri uone na vitukuu.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Nimeshaviona.

**SPIKA:** Amekwishaviona basi na vile vinavyofuata sijui vinaitwaje.

Mheshimiwa Mohamed Rajabu, Msaidizi wa Bunge Sports Club, ameniomba nitangaze kwamba Timu ya Bunge katika safari yake ya Pemba kwenye Sherehe za Mapinduzi mwaka huu, ilicheza mechi na Timu ya Veteran wa Pemba na kama kawaida

Timu ya Bunge ikawafunga magoli matatu kwa mawili. Ameniomba pia nitangaze tukio la aibu kidogo kwamba, Timu ya Baraza la Wawakilishi iliyotualika huko ilituogopa na kushindwa kufika uwanjani kwa kuhisi kwamba wangefungwa magoli zaidi ya matatu.

Kwa hiyo, naomba wenzetu Wawakilishi wasiwe na hofu sana, tutashukuru kama watatupa mwaliko mwingine katika muda usiokuwa mrefu ili tucheze.

Waheshimiwa Wabunge, leo saa tano kamili katika Ukumbi wa Pius Msekwa tutakuwa na Kikao cha Briefing; ni muhimu sana, naomba msichukue muda mrefu sana kwenye chai.

Najua hatujakutana kwa miezi kama miwili na nusu na kwa hiyo kuna kumbukumbu, kuelezana ya Jimbo, lakini tukiwahi saa tano kamili nawahakikishia kabisa kabla ya saa sita tukakuwa tumemaliza briefing na kwa hiyo kusalimiana sasa kunaweza kuendelea vizuri zaidi baada ya hapo. Briefing ni muhimu.

Katika ratiba imepangwa pia kwamba, saa kumi jioni Wabunge watakaa katika mtindo wa *Party Caucuses;* upande wa Upinzani na upande wa CCM; kwa hiyo, imeachwa fursa hiyo ili hilo liwezekane. Kwa maana hiyo basi, haitawezekana kukutana jioni na kwa hiyo naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.40 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 27 Januari, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*